ARUSI

Arusi: Muhtsari wa mafunzo.

Maelezo mafupi -

DARASA LA #1:

I. Utangulizi.
II. Arusi: Masomo ya Kawaida ya Biblia
III. Arusi na Jukumu ya Arusi:
   A. Utangulizi.

DARASA LA #2:

III. Arusi na Jukumu ya Arusi:
   A. Utangulizi (unaendelea)
   B. Mpango wa Mungu wa Maumbile.

DARASA LA #3:

III. Arusi na Jukumu ya Arusi:
   B. Mpango wa Mungu wa Maumbile (unaendelea).
   C. Ni Juku mu gani Zina tendeka katika Arusi?

DARASA LA #4:

III. Arusi na Jukumu ya Arusi
   C. Ni Juku mu gani Zina tendeka katika Arusi? (zinaendelea).

DARASA LA #5:

III. Arusi na Jukumu ya Arusi:
   D. Kufanana kwa Uhusiano wa Arusi.
   E. Mwisho.
   Mtihani

ARUSI

Maelezo mafupi

Mtihani

Maswali yanayoweza kupewa Pointi 20

1) Kusimamia kweli kwamba wanawake ni sawa na wanaume kwa kufuatana na maumbile (kurasa 244, 245).

2) Ni nini kutii kwa mke Kibiblia (Kurasa 259-262)?

3) Fafanua jukumu ya mwanamume Kibiblia (Kurasa 265-267).

Maswali yanayoweza kupewa Pointi 10

1) Taja moja ya makusudi ya Mungu ya arusi. Tia Andiko linaloweza kutazamwa (ukurasa 242).

2) Uhusiano wa arusi ni mfano wa . . . ? Peana mifano miwili (Tia andiko linaloweza kutazamwa; Ukurasa 243).

3) Tuna maana gani tunapotumia neno "daraka" kueleza jukumu la arusi (ukurasa 249)?

4) Nini "himizo sawa" katika aruisi (ukurasa 254).

5) Eleza kwa sentensi moja au mbili tofauti baina ya "50/50" ya upendo na upendo "100/100" (uk. 264).

6) Tumia mawazo ya kutambulikana na jukumu zinazohusiana katika Utatu kama kufanana kwa mawazo ya kutambulikana na kuhusiana kwa jukumu za arusi (uk. 271).

ARUSI

Maelezo mafupi

I. Utangulizi

A. Umuhimu wa Aruisi.

1. Hali ya msingi kabisa ya ujamaa ni jamaa.

   a. Hali ya msingi ya uhusiano wa jamaa ni uhusiano wa arusi. Uhusiano baina ya mume na mike ndio uhusiano wa mwadamu ulio wa msingi kweli.

   b. Arusi ilikuwa uhusiano wa mwanzoni wa mwanadamu kama ulivyoanzishwa na Mungu katika shamba la Edeni.

2. Imesemwa kwamba arusi si kutafuta yule mnaweza kuishi naye, lakini ni kutafuta mtu ambaye huwezi kuishi bila yeye.

   a. Msemo huu unatia mkazo wanguvu za Mungu kwa kutia watu wawili pamoja.

   b. Unatia mkazo pia umuhimu wa arusi. Arusi inatumika kukamilisha mwingine. Hakika, kulingana na Andiko, mwanamke ali umbwa kama "msaidizi" au kukamilisha mwanamume (Mw. 2:18).

B. Yaliyomo katika Kosi Hii.

1. Kwanza, tutapeana kifupi, funzo la kaawaida la Biblia juu yalengo la arusi.

2. Pili, tutaji funza zaidi hasa fikira ya jukumu la arusi kufahamu yalae Biblia huse ma juu ya arusi na uhusiano baina ya mume na mke.

ARUSI

Maelezo mafupi –

II. Arusi: Mafunzo ya Kawaida ya Biblia.

A. Funzo la Mwa. 2:18-24.

1. Kwanza twaona Mungu alifanya "msaidizi" wa mume (Vif. 18-22).

   a. Neno la kiebrania linalotafsiriwa "msaidizi" ni neno lenye maana ya "kukamilisha au kujaza."

   b. Hivyo ni, mwanamke ni kamilisho la mwanamume Anamjaza na kumkamilisha.

2. Katika Kif. 23, twaona majibu ya kiumbe hiki "msaidizi".

   a. Lengo ni kwamba mwanamume na mwanamke kwa asili wana husiana kwa sababu mwanamke alitolew kwa mwanamume.

   b. Uhusiano ni wa asili na wa kukaribiana.

3. Mwisho, katika kif. 24, twaona tekelezo la kweli la kuimarisha arusi.

   a. "Kwa hiyo:" Uwepo wa kuimarisha arusi unajengwa juu ya chaguo la Mungu kama Mungu Mwumba.

      1) Arusi inaimarishwa kwa sababu ("kwa hinyo") ya vile Mungu aliumba mwanamume namwanamke.

      2) Kwa vile Mungu aliumba mwanamke kutoka kwa mwanamume, kuna arusi. Ni ya kufikiriwa, ya asili, na ya karibu.

   b. "Mwanamume atamwacha baba yake na mama yake:" Mwanamume ana chukua jukumu.

      1) Lazima aache jamaa yake ya asili kuanza jamaa mpya.

      2) Wajibu wake mpya lazima uwe kwa jama hii mpya.

Maelezo mafupi

c. **"Naye ataambatana na mkewe:"** Mwauzo mpya una mwanamume na mwanamke pamoja.

1) Mwanamume aache na aambatane. Hivyo ni kusema, lazima aache nyuma ya zamani na aambatane na mpya.

2) Neno "kuambatana" maana yake ni fikira ya kudumu. Huu si mpango hivi hivi. Ni uhusiano wa kudumu wa nguvu.

d. **"Nao watakuwa mwili mmoja:"** Matokeo ni kwamba mwanamume na mwanamke huwa wameungana hivi kwamba huonye sha mpango wa asili wa uumbaji. Mwanzoni na kulingana na maandiko walikuwa mmoja (kwa sababu mwanamke alitolewa kutoka kwa mwanamume).

1) Matumishiya neno "kuwa" hapa yalenga kule tungeita maendeleo ya arusi. Hivyo ni, uhusiano unajengwa. Unafanyiwa kazi, umekuwa mzuri zaidi, na kukamilishwa kwa muda.

2) Fikira ya "mwili mmoja" maana yake ni uhusiano wa arusi huunda kuju likana kumoja. Pia kunalenga kukmilisha kugusana kimwili kwa uhusiano wa arusi. Kawaida sana sana, kunalenga muungano na uhusiano wa upendo.

3) Neno "Nao" ni la muhimu sana. Ijapokuwa wanaku wa mwili mmoja kupitia uhusiano wao, wana fanya hivyo kana "nao". Hivyo ni, wao ni wawili, walioungana hata hivyo wana onekana, pamoja hata hivyo kama mmoja mmoja binafsi.

4) Hili litakuwa la muhimu kuweka fikirani tutaka-poanza kusema juu ya jukumu za ndoa katika sehemu nyingine ya kosi hii.

4. Mwisho wa Masomo yetu ya Biblia.

a. Uhusiano wa ndoa ulianzishwa na Mungu.

b. Ni mwanzo au msingi wa uhusiano wa binadamu wote.

ARUSI

Maelezo mafupi –

Mahali pa Majadiliano

Jadili shida nyingine za siku hizi katika arusi zinazohusiana na kutokufahamu mawazo yafuatayo:

- msaidizi/kukamilisha
- acha/ambatana
- anao wanakuwa mwili mmoja

B. Makusudi ya Mungu Kwa Arusi.

1. Arusi inatumiwa kama njia ya kuonyesha mfano wa Mungu. Utatu wa Mungu (Mwa. 1:26) ambaye anafanya kazi kwa umojana umoja unamfanya mtu (ambaye ni mwanamume na mwanamke: Mwa 1:27 na 5:1). Kwa Mfano wake mwenye we ambaye lazima afanye kazi kwa umoja na Shirika.

2. Arusi ilifanywa kuzidisha mzao mwenye kumcha Mungu (Mwa 1:28; Mal 2:14, 15).

3. Arusi imefanyawa kuwa sehemu ya njia ambayo mtu atatawala viumbe wa Mungu (Mwa 1:28).

4. Arusi imefanywa ili mtu na wanawake kwa umoja waweze kukamilishana (Mwa 2:18-24).

5. Arusi huonyesha uhusiano wa Kristo na kanisa (Efe 5:23-32).

6. Arusi hutumiwa kurunja moyo tabia ya zinaa (1 Kor 7:2, 9).

7. Arusi inakusudiwa kuletakutosheka kulikokamilika (Mith 5:19).

ARUSI

Hali za Aruisi:

Ufafanuzi wa uhusiano wa arusi:

Lazima iheshimiwe (Ebr 13:4).
Iwe ya kudumu (Mt 19:6).

Uhusiano wa arusi ni mfano wa:

Mwungano wa Mungu na Israeli (Is 54:5).
Muungano wa Kristo na Kanisa (Efe 5:23-32).

Sherehe ya arusi:

Yesu alitambua udhibitifu wake (Yn 2:1-11).
Ina linganishwa na furaha (Yer 7:34).

Maelezo mafupi

III. Arusi na Jukumu za Arusi.

A. Utangulizi.

1. Umuhimu wa arusi. Kufahamu jukumu ya arusi, lazima kwanza turudie umuhimu wa arusi.

   a. Tumekwisha kuonyesha kwamba arusi ilianzishwa na Mungu Mwenyewe (Miva 2:18, 24). Haikuv umbuliwa na mtu.

      1) Ilianzishwa kwa sababu ilikuwa ya muhimu (Mwa 2:18, 20).

      2) Ilianzishwa iendelee (Mwa 2:22-24).

         a) Kuendelea kumeanza wakati Mungu mwenyewe ali waleta wale wawili pamoja (kif. 24).

         b) Mwungano wa msingi wa jamaa una simamiwa na mwungano wa jamaa (kif. 24).

         c) Ni uhusiano wa kudumu (mwili mmoja kif. 24).

Maelezo mafupi –

b. Arusi huleta njia ya mwanamume kuwa mkamilifu (rudia tuliyosema juu ya mana ya neno "msaidizi".)

1) Kufanana kunakopatikana katika Efe. 5 kunaajiza uhusiano ulio wazi baina ya Kristo na mume na mwili wa kanisa na mke.

2) Tukiwa na haya fikirani, soma Efe 1:23.

a) Mwili ni "ukamilifu" wa Kristo.

b) Tukitumia kufanana kwa Efe. 5, Tungeweza kusema kwamba mke ni "ukamilifu" wa mume. Hivyo ni, kumkamilisha. (tazama vile hii inakubaliana na maana ya neno "msaidizi").

Mahali pa Majadiliano

Shirikianeni shuhuda za jinis arusi imeleta ukamili fu kwenu ninyi mliooa au kuolewa.

2. Kujiona wa chini kinyume cha usawa. Wanawake ni wa chini kwa wanaume. Wao ni sawa nao.

a. Wanawake ni sawa na wanaume katika kuumbwa.

1) Mungu aliumba mwanamune. Pia aliumba mwanamke. Mungu alihusika hasa na sawa katika viumbe wote wawili.

2) Mwanamke hakuumbwa na mwanamume (mwanamume alikuwa amelala alipokuwa anaumbwa). Mwanamke aliumbwa kutoka kwa mwanamume Aliumbwa na Mungu.

3) Tofauti baina ya wanaume na wanawake msingi wake ni juu ya mpango wa Mungu wa kuumba.

Maelezo mafupi

4) Usawa wa wanaume na wanawake msingi wake ni kweli kwamba wote wawili wana Mwumba mmoja.

a) Mtu yuko chini ya Mungu kwa sababu Mungu alimwumba.

b) Chungu kiko chini ya mfunyanzi kwa sababu mfinyinzi alikiumba.

c) Kutofahamu na kusema mwanamke yuko chini ya mwanamume hutokana na kutofahamu kuhusu ni nani aliyemwumba mwanamke. Mwanamume hakumfanya mwanamke. Mungu alimfanya mwanamke. Mwanamume na mwanamke wana Muumba mmoja.

Mahali pa Majadiliano

Tumia fikira za awali kujadili kweli kwamba wanawake ni sawa kabisa na wanaume katika kuumbwa. Ni mipaka gani iliyoko katika utamaduni wako unaopinga kuonekana wazi huku?

b. Wanawake wako sawa na wanaume katika kuendelea kuweko kwa vizazi.

1) Soma 1 Kor 11:11, 12.

2) Kama mtu mmoja humtegemea mtu wa pili kuishi, basi mtu wa pili hawezi kufikiriwa wa chini. Wote wawili ni sawa na wana tegemeana.

a) Hii ni kweli katika wote wawili wanaume na wanawake. Wanategemeana waweze kuendeleza katika vizazi.

b) Wanawake wawili hawawezi kuendeleza vizazi. Wanaume wawili hawawezi kuendeleza vizazi. Inachukua mwana mume na mwanamke. Wanate gemeana waweze kuishi, na kwa hivyo wao ni sawa sawa.

c) Tofauti iliyoko kuhusiana na madaraka yaliyoko baina ya mwanamume na mwanamke msingi wake si juu ya kuwa sawa, lakini ni juu ya vile wanavyohusiana katika jukumu zao.

Maelezo mafupi -

3) Wanaume na wanawake ni sawa sawa katika kufanana kabisa.

4) Wao ni tofauti katika jukumu zao. Kusema kwamba wanawme na wana wake ni sawa sawa maana yake si kusema kwamba wanafanana.

c. Kosa la mafunzo ya "kuwa chini kwa wanawake" msingi wake ni kukata shauri kubaya bila sababu nzuri.

1) Walimu wa Kiebrania wa zamani walisema kwamba wanawake walikuwa wa chini kwa sababu Hawa alifanywa kutoka kwa Adamu. Aina ya kweli kama hii maana yake ingekuwa wanaume wako chini ya mavumbi kwa sababu Adamu aliumbwa kutoka kwa mavumbi!

2) Walimu wa Kiebrania wa zamani wali sema pia kwamba wanawake walikuwa chini ya wanaume, kwa sababu Hawa alifanywa baada ya Adamu.

a) Kama hivyo ni kweli, mtu yuko chini ya wanyama walioumbwa mbele yake?

b) Kusema kweli, kweli kwamba mwanamke alifanywa kutoka kwa mwanamume huimarisha usawa wake naye. Yeye, kama Adamu alivyotangaza, mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu. Wao ni sehemu ya kila mmoja na kwa hivyo wako sawa sawa katika kufanana kabisa.

c) Tena, hiyo haikatia tofauti zao. Mwwanamke alifanywa kutoka kwa mwanamume na baada ya mwana mume. Kuna mpango wa Mungu wa vitu. Hivyo, kuna mpango wa Mungu katika uhusiano baina ya mwanamume na mwanamke. Huu ni msingi wa "jukumu" za arusi.

Mahali pa Majadiliano

Utamaduni au dini yako imefundisha kwamba wanawake ni wa chini? Kama ni hivyo, uko tayarikusaidia kurekebisha njia hii yakufikiri? Waweza kuanza kanisani. Jadili jambo hili.

Maelezo mafupi –

d. Yesu alipinga kweli hii mbaya wakati wake, lakini hangekuwa wakili wa chama cha siku hizi cha kuwaweka huru wanawake ambacho kina nguru katika Ulimwengu wa Magharibi.

1) Yesu aliwakemea Mafarisayo wenye hali mbili zilizofanywa na ubaguzi wao na hukumu kinyume cha wanawake (tazama Mt 5:28).

2) Alifanya hivyo kwa sababu aliwatazama wanaume na wanawake kama kuwa sawasawa kuhusikana dhambi.

3) Hata hivyo, hakuwa wakili wa "kuwaweka huru wanawake" kama inavyosemwa leo katika Ulimwengu wa Magharibi.

4) Alielewa kwamba wanaumena wanawake ni tofauti.

a) Chama cha siku hizi cha kuwaweka huru wanawake hasa chawaza uhuru kinyume. Ili mwanamke aweze kuwekwa huru, lazima awekwe huru kama mwanamke. Kuwa huru kutokuwa mwanamke si uhuru hata kidogo.

b) Chama cha uhuru wa wanawake hakitaki kufanya wanawake kuwa sawasawa na wanaume. Kinataka kuwafanya wanaume na wanawake kuwa sawasawa.

c) Wanaume na wanawake wako sawa sawa. Wao si sawasawa. Kama vile haya yalivyodhahiri haionekani na ulimwengu usio na maana, wenye dhambi (tazama Rum 1:18-32).

Mahali pa Majadiliano

Ni kwa njia gani chama cha siku hizi cha uhuru wa wanawake (hasa kama vile kimevutia katika Ulinwengu wa Magharibi) kimeonekana kusaidia na kuumiza jikumu halisi ya wana wake wa siku hizi.

Maelezo mafupi

5) Wanawake ni sawasawa na wanaume katika Kristo.

6) Ni utu u ulioanguka uliounda hali ya kuwa chini ya wanawake. Tangu mwanzo wa uumbaji haikuwa hivyo.

a) Ukombozi umerudisha utu ulioanguka katika kusudi lake la asili. Uhuru wa watu unaonekana katika kusudi la asili la Mungu. Hivyo, katika maana ya kweli, Kristo aliwaweka huru wanawake.

b) Anakomboa fikira za mwanamume kuweza kufahamu usawa wa wanaume na wanawake anapotumia sawa tofauti baina ya wanaume na wanawake.

e. Tumeona kwamba tofauti baina ya wanawake na wanaume haipatikani katika kufanana kwao kabisa (kufanana kwao ni katika Kristo). Tofauti baina ya wanawake na wana ume inapatikana mpango wa uhusiano mkuu wa Mungu ambao ulianzishwa katika uumbaji.

Discussion Point

Tumia Maandiko yafuatayo kuja dili jinsi Biblia inaonyesha usawa wa wanaume na wanawake: Mwa 5:1, 2; Mwa 1:27; Mwa 3:28; Efe 5:28; na 1 Pt 3:7.

B. Mpango wa Mungu wa Maumbile.

1. Ndiyo, mume na mke wako sawasawa katika hali ya kufanana kabisa. Sasa lazima tuulize: Wana husianaje?

a. Jamaa ni msingi wa umoja wa jamii.

b. Katika mpango wa jamaa, mke amtii mume na watoto wawatii wazazi. Kuna mpango wa Mungu wa mamlaka.

1) Lazima turudie kwamba ume, mke, na watoto ni sawasawa katika fikira ya kufanana kwao kama wanadamu.

2) Wako tofauti katika vile wanafanya mambo katika jamaa (jukumu).

Maelezo mafupi

c. Katika mpango wa Utatu, Baba ana madaraka fulani juu ya Mwana na Roho ijapokuwa wote watatu ni sawasawa na Mungu. Hivyo ni, wao ni sawasawa katika kufanana kabisa na tofauti katika kazi au jukumu. Kama ilivyo katikajamaa, Utatu una mamlake ya mpango uliowekwa na Mungu.

Mahali pa Majadiliano

Tumia mchoro ufuatao kujadili mpango wa maumbile. Fikiria 1 Kor 11:3 kuhusiana na mpango wa maumbile na mchoro ulio hapa chini.

Sawasawa katika: kufanana kabisa	Tofauti katika: kazi/Jukumu/Mpango wa kuhusiana		
Mwanamume = Mwanamke = Mtoto	Mwanamume || Mwanamke || Mtoto	1 Kor 11:3 Efe. 6:1	Mpango wa Mamlaka
Baba = Mwana = Roho Mtakatifu	Baba || Mwana || Roho Mtakatifu	Yn 3:16 Matendo 13:33 Yn. 15:26 Yn. 16:14	Mpango wa Mamlaka

2. Tuna maana gani tunapotumia neno daraka?

   a. Daraka haliangalii vile mwanamume na nwanamke wanavyostahili. Linatazama mahali ambapo kila mmoja anachukua kulingana na mpango ulioanzishwa na Mungu.

   b. Daraka halihusiki na hali ya chini au ya juu kwa sababu ni daraka la kazi. Si daraka la ukuu au kustahili.

   c. Daraka haliangalii daraka la kazi na mpango kwa sababu ni daraka la wajibu na mamlaka ambayo yalianzishwa katika uumbaji.

ARUSI

Maelezo mafupi –

Tia Maelezo Yako:

3. Jifunze Efe 5:22-24.

   a. Paulo anasema kwamba mume ni kichwa cha mkewe. Hasemikwamba mume yuko mbele ya mkewe.

      1) Mume ni kichwa katika kazi na pa kuhusiana.

      2) Hayuko mbele katika kuwa mkuu na kufanana kabisa.

   b. Katika Efe. 5 Paulo azungumza juu ya kazi mbili tofauti za wana damu wawili walio sawasawa.

      1) Hivyo, kazi za mume na za mke ni tofauti, si kwamba haziwezi kulinganishwa. Kifupi kwa sababu zinatofautiana na zina kazitofauti katika mpango wa Mungu maana yake sikwamba hazilingani.

      2) Tena, sababu yake ni kwa vile wanaume na wanawake wakatie ule ule wako sawa sawa na tofauti.

         a) Kusema mmoja yuko chini ya mwingine ni kosa la kawaida la wanaume wenye kiburi na wasio na haki.

         b) Kusema kwamba mmoja ni sawasawa na mwingine ni kosa linalofahamika na wote la wasi na wanawake waliotatanishwa (wanaoonekana mara nyingi katika chama cha kuweka huru wanawake katika Ulinwengu wa Magharibi).

ARUSI

Tia Maelezo Yako:

Maelezo mafupi

4. Marudio Mwa 2:18-24.

   a. Tumekwisha kujifunzakifungu hiki kuona usawa wa mume na mke. Sasa lazima tuone vile mume na mke wako tofauti.

   b. Daraka la kazi ambalo lime fafanuliwa hapo awali si matokeo ya kuanguka kwa mtu. Ni matokea ya uchaguzi na mpango wa Mungu katika uumbaji. (1 Tim 2:13).

      1) Mwanamke alifanywa kutoka kwa mwanamume.

      2) Mwanamke alifanywa kwa ajili ya mwananume.

      3) Mwanamke amepeanwa kwa mwanamume.

      4) Mwanamke amepewa jina na mwanamume.

ARUSI

Maelezo mafupi –

5. Maelezo ya mwishoni.

   a. Hivyo, kukomboa uhusiano katika arusi hakupingi tofauti ya kazina jukumu la mume ne mke. Badala yake, kunatengeneza utendaji wa kazi tena, baada ya kuharibiwa na jamii iliyoanguka.

      1) Wakati kazi na jukumu ni nzuri, basi arusi ni nzuri. Bila kuwa na ufahamu na mazoezi ya kazi au jukumu hizi, jamaa itaingia katika mchafuko. Itakosa mpango na umoja.

      2) Ndiyo, lazima pawe na mpango katika jamaa. Mtu fulani lazima aongoze. Madaraka haya ya wongozi yame peanwa wazi kwa mume na baba. Mamlaka yake lazima yakubaliwe.

   b. Hitaji hili la mpango ni kweli katika aina nyingine zote za shirika./ Fikiria mfano wa kanisa la mtaa.

      1) Kuna aina ya daraka la kazi katika kanisa la mtaa.

         a) Mshirika wa kanisa ana hoja ya kumtii pasta (1 Kor 16:16; 1 Thes 5:12, 13; Ebr 13:7).

         b) Wakati huo huo pastor au kiongozi lazima awatumikie binafsi na ajitolee kwa washirika wa kanisa (tazama 1 Kor 16:15, 16).

      2) Kuna daraka fulani la kazi katika jamaa.

         a) Mke amtii mume we (Efe. 5:21,22). Jambo la ku shangaza, neno hilo hilo katika kiyunani (upotaso) limetumiwa katika 1 Kor 16:16 ku fahamu kutii kwa mshirika wa kanisa kwa kiongozi wa kanisa,kama lilivyotumiwa katika Efe. 5:21,22 kufafanua kutii kwa mke kwa mumewe.

         b) Wakati huo huo mume apaswa kumtumikia binafsi, kumpenda, nakujitoa kwa ajili ya mkewe (Efe 5:25).

      3) Kila aina ya ushirika lazima uheshimu sehemu hizi za uhusiano ili ushirika udumu nakufanya kazi sawasawa.

Maelezo mafupi

4) Kiongozi wa kanisa na mshirika wa kanisa ni tofauti katika muundo na utendaji wa jukumu kani sani. Hata hivyo, wao ni sawasawa katika kufanana kabisa kwa sababu kufanana kabisa kwao ni katika Kristo.

5) Mume na mke ni tofauti katika muundo na utendaji wa jukumu katika jamaa. Hata hivyo, wao ni sawasawa katika kufanana kabisa kwa sababu kufanana kabisa kwao ni katika Kristo.

   a) Mume na mke lazima wafahamu u sawa wao.

   b) Inawapasa wafahamu pia kwamba wao ni tofauti nawote wawili lazima wamtii Kristo kwa kumtumikia ndani ya mpango wa utendaji wa jukumu uliopangwa na Mungu.

Tia Maelezo Yako:

Mahali pa Majadiliano

Tumia mawazo ya hapo awali kuendeleza majadiliano na ujibu maswali.

Maelezo mafupi –

C. Jukumu za utendaji ni gani katika Arusi?

1. Nia Sawa.

   a. Amri ya kujazwa Roho na kunyenyekeana katika kicho cha Kristo (Efe. 5:18,21) hutenda kama utangulizi katika maelezzo ya Paulo ya jukumu za arusi katika Efe 5:22-33.

   b. Utangulizi huu hutia lengo juu ya ni nani aliye chini ya Kristo, si juu ya nani aliye juu ya nani.

      1) Jambo ni kwamba mume na mke lazima wahusiane kulingana na kutaka kwa Kristo.

      2) Lazima watii mundo wa mpango Wake. Nia sawa yenye heshima kwa utendaji katika jukumu halisi ya arusi ni kutii Kristo.

         a) Mume ambaye hampendi binafsi, kumtumikia na kumwongoza mkewe hukosa kumtii Kristo.

         b) Mke ambaye hamtii na kumheshimu mumewe hukosa kumtii Kristo.

   c. Kama hatukubali kunyenyekea na kutii Kristo kuwa nia sawa, kisha tutaanza kulenga juu ya madaraka ya mwenzetu.

      1) Tutaanza kufanya jukumu zetu kutegemea kumaliza jukumu la mwingine.

      2) Tutaanza kulenga juu ya "haki" zetu katika arusi zetu, badala ya juu ya madaraka yetu katika arusi zetu.

      3) Haya yote huongoza kwenye wa kuji penda na usio wa kweli.

      4) Katika arusi nzuri, mume na mke wanacho chewa kutenda katika jukumu zao kwa madaraka ya jukumu zao, wala si kwa madaraka ya jukumu zao.

      5) Zaidi ya yote, wana chochewa na tamaa yao ya kumtii na kumpendeza Kristo.

Maelezo mafupi

2. Jukumu la mke ni **kunyenyekea**.

   a. Umuhimu wa kunyenyekea kwa mke.

      1) Ajifunze kwa kutii (1 Tim 2:11).

      2) Agunze juu ya kutii (Titus 2:5).

      3) Ahubiri katika kutii kwake (1 Pt 3:1).

   b. Lile kutii silo.

      1) Kutii si "utumwa".

      2) Kubadilisha kwa 'kutii' ni matokeo ya kuanguka kwa mwanamume shambani.

Mafunzo Ya Biblia Ya Mwandishi:
Mafunzo ya Biblia ya Mwa 3:16 na Mwa 4:7.

Mafunzo ya Biblia ya Mwa 3:16 na Mwa 4:7. Nini maana ya neno "tamaa?" (tazama: Neno la Kiebrania kwa "tamaa" ni "teshuka" na hapa ndipo mahali pawili katika kitabu cha Mwanzo ampapo tunapata neno hili).

Kwanza, lazima tuone kutoko 4:7 kwamba si "wazi" yenye maana ya "tamaa". Tafsiri inayofanya sawasawa na tamaa katika 3:16 na tamaa ya mwili wa mwanamke kwa mumewe pengine ni matokeo ya yote mawili fikira za kutamani (katika sehemu ya mwanamume) na mafunzo mabaya ya Biblia.

Kuangalia kwa makiri maandiko, neno "tamaa" ni"kinyume" cha wazo. Katika 4:7, limetumiwa hapo kwa "tamaa" ya dhambi kutawala. Katika 3:16, twaweza kumalizia kusema kwamba "tamaa" ya mwanamke si iliyowekwa mwanzoni (kumbuka, hii ni sehemu ya adhabu au laana ya kuanguka). Mke alikwenda kinyume cha jukumu lake la asili la kutii shambani alipochukua sehemu ya wongozi kulingana na Tunda la mti walioonywa juu yake. Hivyo, amke anaadhibiwa sasa kwa kutamani kumtawala mumewe.

ARUSI

Maelezo mafupi -

Mafunzo ya Biblia ya Mwandishi:

Tafsiri ya M wa 3:16 na Mwa 4:17:

Pili, kama vile Bwana anamwambia Kairi katika 4:7 aishiride au aitawale dhambi, vivyo pia amwambia mume katika 3:16 amtawale mkewe. Kutii kwa asili kunabadilishwa kwa nguru kutiii ambako si kwa asili. (Kumbuka: haya ni matokeo ya maanguko ya binadamu na maanguko ya mwanadamu yanakombolewa na Kristo).

Matokeo na uharibifu wa maanguko ni wazi. Sivyo Mungu alikusudia (kumbulea: kwa ukombozi laana hii yaweza kukombolewa). Maanguko yameharibu kutii kwa kutaka kwa mke kwa kuifanya tamaa ya kutawala mume.

Yameharibu pia uongozi wa upendo wa mume kwa kuufanya utawala wa utumwa au utumwa.

Kama tukiendelea na kulinganisha 3:16 na 4:7, basi tungeweza kusema kwamba kama mume akifanya "vyema" (hivyo ni, kama akimpenaa mkewe kama vile Kristo alipendavyo Kanisa); basi mke hatakuwa "anainama mlangoni" au kujaribu kumtawala.

Hii ni kweli ya muhimu katika majadiliano yetu ya uhusiano wa arusi. Ni ya sili sana. Dhambi huyafanya yasiwe ya asili. Kama mume ampenda mke kama impasavyo, basi itawezekana zaidi kwamba patakuwa na majibu ya asili ya mke kuwa katika kutii. Kinyume ni kweli pia. Kama mke atamtii mumewe basi itawezekana zaidi kwamba patakuwa majibu ya sili kwa mume kupenda mkewe.

Maelezo mafupi

3) Adhabu ni kuishi maisha yasiyo ya asili. Ni kwenda kinyume cha kule maji yanadekea au kukata kinyume cha mbegu ya mti. Ni kupingana na yaliyo ya asili.

   a) Katika nia hii Mungu hatuadhibu hata kidogo. Twajiadhibu wenye we kwa kutotii na vivyo kupata matokeo (tazama kanuni hii katika Yn 3:18, 19).

   b) Hii ni kweli ya maisha. Dhambi matokeo yake ni adhabu siyo sana kwa sababu Mungu huturudi (ijapokuwa huturuki: tazama Ebr. 12:4-11), lakini kwa sababu kwenda kinyume cha Mungu (kutenda dhambi) ni kwenda kinyume cha maumbile na yaliyo ya asili. Hii matokeo yake katika hutia uchungu juu yako mwenyewe kwa kufanya jambo kwa njia (lisilo la asili) ya makosa. (Rum 6:23; Jn 3:18, 19).

Maelezo ya Mwandishi:

Kufanana #1: Kama unapigilia mshumari na utie kidole chako juu ya kichwa cha msumari, basi utasikia uchungu. "Adhabu" hii si kutoka kwa Mungu ambaye kwa wakati huo alikata shauri kukufanya ulipe kwa sababu ya kosa lako. Nimatokeo ya kufanya jambo kwa njia ya makosa.

Tia Maelezo Yako:

ARUSI

Maelezo mafupi

Maelezo ya Mwandishi:

Kufanana #2: Kama unacheza mpira wa miguuu na ukijaribu kupata goli na unakimbia mbele ya mpira na wachezaj: wa upande ule mwingine unaocheza nao, basi mpiga filimbi atasema umekwenda "ofsaidi". Utalipizwa na mpiga filimbi kwa sababu ulifanya jambo la makosa. Mpiga filimbi hakuadhibu wewe. Unajiadhibu mwenyewe.

Tia Maelezo Yako:

Maelezo ya Mwandishi:

Kufanana #3: Ugonjwa wakufisha unaoitwa UKIMWI si sana hukumu ya Mungu kinyume cha wenye kdhambi kama vile ilivyo matokeo ya kufanya mambo kinyume cha mpango wa asili wa maumbile ya Mungu. Mungu si sana kumikumu au kuadhibu mtu ambaye maisha yake anaishi katika makosa ya uzinifu. Mtu huyo hujiadhibu mwenyewe kwa kwenda kinyume cha mpango wa Mungo: kwa kweli, kwa wakatia huu, twajihukumu (fikiria Yn 3:18, 19; 1 Kor 11:31; Mt 7:1, 2).

Tia Maelezo Yako:

c. Kutii kwa kibiblia na gani?

Maelezo mafupi

1) Ni kutegemea.

a) Katika Efe 5:21-24 Paulo atunia wazo la mwili wa Kristo (ambao alikuwa amekwisha kueleza katika Efe 1:22, 23; 4:15, 16) kueleza wazo la jukumu la arusi.

b) Ni ya kupendeza kwamba katika 4:16 Paulo atumia Neno la Kiyunani "epichoragia" (linalotafsiriwa kama "kupeana mahitaji") kuonyesha kwamba mwili unapata kulishwa, maisha na mwongozo kutoka kwa kichwa. Neno hilo hilo lilikuwa neno la ujuzi lililotumiwa wakati huo kuonyesha yanayompasa mume kupeana mahitaji ya msingi kwa mkewe.

c) Tunapofikiria kufanana kwa mwili wa Kristo ambako Paulo anatumia kufafanua jukumu ya mke ya kutii katika Efe 5, twawe zakuunganisha na Efe 4:16. Sehemu ya muhimu ya kutii ni kukubali na mazoezi ya nia ya kutegemea.

d) Mke anayemtegemea mumewe hapingani na asili. Katika Mwa 2 tuliona vile uumbaji wa mwanamke ulitegemea kuumbwa kwa mwanamume.

Tia M aelezo Yako:

Tia Maelezo Yako

Jadili kutii kibiblia katika kuangalia jamii ya kisasa na mzigo wa usumbufu wa wanawake kuajiriwa nje ya nyumbani (katika utamaduni wa Magharibi).

Maelezo mafupi

2) Ni kuwa chini

a) Tena, twaweza kufikiria kufanana kwa mwili wa Kristo kuwa chini ya Kichwa.

b) Huku kuwa chini kunaungana na upendo kwa Kichwa na kumzalia matunda (uinjilisti, ushuhuda mzuri na sifa, niki).

c) Twaona matendo kama haya haya katika kutii kwa mke ambaye anatajwa katika Titus 2:4, 5.

(1) Anampenda mumewe (kif. 4).

(2) Ana akili na safi (kif. 5: humpatia mumewe sifa njema).

(3) Hufanya kazi nyumbani mwao (kif. 5: anamletea mapato mumewe).

d) Twaona matendo haya haya pia katika Mit. 31 ya mwanamke. Analeta mapato na kumletea mumewe sifa nzuri (tazama vif. 11, 12, 15, 18, 23).

Tia Maelezo Yako:

Mahali pa Majadiliano

Tumia mawazo ya awali kujadili kuwa chini Kibiblia.

Maelezo mafupi

3) Ni heshima na kustahili mume wako.

a) Soma Efe 5:33.

b) Sehemu muhimu ya kutii ni kuonye sha heshima.

c) Katika siku za Paulo, hili lilifanywa na wake kama matakwa ya sheria. Kutii kwa mke Mkristo lazima kuwe zaidi ya huku. Lazima kunyenyekea, halisi, na lazima kuletwe na kumcha Kristo na mpango wake wa vitu.

d) Inatazamwa katika yaliyomo ya Wakristo, kwa kawaida, kumtii "mmoja na mwingine katika kichwa Kristo". (Eph 5:21).

Tia Maelezo Yako:

Mahali pa Majadiliano

Ni kishindo cha namna gani kinachompata mume anapojua kwamba mkewe hamheshimu? Au ajibuje wakati mkewe anami na hata kuonyesha mbele ya watu?

Maelezo mafupi -

d. Maelezo ya mwishoni juu ya Kutii.

1) Mke anapaswa kufahamu kutii kwa mpango wa Mungu. Anapaswa kukuona kama njia ambayo aweza kudhania mahali pake palipowekwa na Mungu.

a) Hivyo, kutii kwake lazima msingi wake uwe juu ya uhuru na upendo, na si juu ya kuamriwa na uoga.

b) Kwa kweli, Kanisa haliambiwi kwa nguvu kutii. Linatii kwa kutaka kwake lenyewe na kutaka kuwa mtiifu kwa kichwa.

c) Linalostahhili, mke kumtii mumewe kuletwe na msingi wa kicho cha Mungu (Efe 5:21). Hivyo ni, lazima msingi wake mwe juu ya kutamani kumtii Mungu.

2) Mke afahamu na akubali kwamba kutii kwake mumewe hakuwezi kutegemea kutaka kwa mumewe kutimiza jukumu lake.

a) Kutaka kufanya hivyo lazima kuwe safi Hivyo ni, lazima msingi wake uwe katika kutamani kumpendeza Kristo. Macho yake yawe juu yake, na si juu ya mumewe.

b) Kama ma cho yake yako juu ya mumewe, basi ataanguka kwa sababu mumewe ataanguka. Kutii kwake hakuwezi kutegemea matendo ya mumewe.

c) Kama macho yake yako juu ya Kristo, basi hataanguka kwa sababu Kristo haanguki. Kutii kwake kuwe bila masharti.

(1) Kunapaswa kuletwa na kutamani kwake kufanya katika mpango wa Mungu.

(2) Kunapaswa kuletwa na kutamani kuwa mwenye haki (kusimama mahali sawa mbele ya Mungu).

Maelezo mafupi –

3) Hapa twaweza kuimarisha kanuni kuu kwa arusi nzuri. Mume na mke lazima walenge wajibu wao wenyewe badala ya wajibu wa wengine (Mt 7:3-5).

   a) Jambo la kushangaza juu ya sehemu hii ni kwamba kama likitumiwa, mara nyingi litarekebisha arusi isiyo nzuri.

      (1) Kutii kwa mke kwa asili humfanya mume kumpenda na kumwongoza.

      (2) Kupenda na kuongoza kwa mume kwa asili humfanya mke kumtii.

   b) Arusi isiyo nzuri mara kwa mara ni matokeo ya mume au mke ambaye hulenga wajibu wa mwingine badala ya kulenga juu yake au juu wa wajibu wake.

      (1) Wakati haya yanatukia, mume hujaribu kumfanya mkewe kutimiza jukumu la kutii kwa nguvu, naye mkewe anajaribu kumtumia kumwew kutimiza jukumu lake la wongozi kwa kusuki lake biinafsi.

      (2) Hili latukumbusha vile maanguko ya mtu yaliharibu jukumu za arusi (Mwa 3:16 and 4:7).

      (3) Mume kutumia nguvu (amri).

      (4) Mke kufanya kwa kusudi lake binafsi (kutamani kutawala).

ARUSI

Maelezo mafupi -

Maneno ya Mwandishi:

Upendo wa Wakristo na Upendo wa Mwili

Tutazame tofauti baina ya upendo wa ulimwengu, au mwili (unaoitwa upendo "50/50"), na upendo wa Ukristo, au upendo usio na masharti yaani Agape (unaoitwa upendo “100/100”).

Upendo wa kimwili (“50/50”) ni aina ya upendo ambao ni wa kujipendeza mwenyewe. Kila mmoja wao hupeana nusu ya ubinafsi wake wote, au hufanya nguvu 50% katika arusi. Kitu mmoja hupeana akitarajia kwamba yule mwingine lazima apeane sehemu sawasawa na hiyo. Huu kwa kweli ni mafano wa kujipenda.

Yesu alifunua unafiki unaofuatana na upendo wa aina hii Mt 5:46-48.

Upendo wa Ukristo ni "agape" au pendo usio na masharti ("100/100"). Upendo wa aina hii hauna masharti unatendwa kwa ushiriki wa wenzao, bila kujifikiria mwenyewe. Kila mwenzi hupeana ubinafsi wake wote, au 100% ya uwezo wake katika arusi. Kila mwenzihutamani kumsaidia mwenziwe bila kutarajia kutendewa hivyo hivyo, hata wakati kupeana ni kwa matumizi yake mwenyewe na ni ya gharama kubwa.

Pauloafafanua upendo huu katika 1 Kor. 13:5 aliposema kwamba "hautafuti mambo yake."

Arusi ya Ukristo lazima ijae upando "agape" na uzoeze upendo "100/100". Mume na mke wote wa wili lazima watimize jukumu zao bila kutarajia au kutaka kurudishiwa kitu kwa ajili yake. Kusudi lao liwe safi. Makusudi safi ni matokeo ya kuamshwa na Kristo peke yake.

Maelezo mafupi

3. Jukumu la mume ni uongozi.

   a. Maana ya uongozi.

      1) Neno la Kiyunani la "kichwa" ni "kefalay". Linataja mtu aliye na daraka la juu.

      2) Uongozi huonyesha mawazo mawili: mamlaka na mwongozo.

   b. Mamlaka.

      1) Mamlaka si matokeo ya kutawala. Ni matokeo ya kutumika (Mt 23:11).

         a) Wakati mume anatazama mamlaka kama "haki" yake, basi ataanza kuitisha bila kwepuka. Atazoea kutawala badala yakutumika. Matokeo yake yatakuwa arusi mbaya.

         b) Wakati mume anatazama mamlaka atayatendea kazi na kuyapata. Atatumika badala ya kutawala. Matokeo yake ni arusi nzuri.

      2) Mamlaka si matokeo ya kuanguka. Nimatokeo ya maumbile.

         a) Inatupasa tukumbuke kwamba mwanamume alipokea jukumu la wongozi katika shamba la Edeni.

            (1) Adamu alipewa mamlaka ya kuwaita wanyama majina (Mwa 2:19).

            (2) Alimtaja jina mkewe pia (Mwa 3:20).

         b) Katika arusi iliyokombolewa ya Ibrahimu na Sara, Ibrahimu alizoea mamlaka haya. Katika maandiko juu ya kuti kwa mkena mamlaka ya mume, twaona kwamba Sara alimwita Ibrahimu "bwana" (tazama 1 Pt 3:1-6).

Maelezo mafupi

Tia Maelezo Yako:

c. Mwongozo.

1) Msimamo wa mwongozo katika wongozi wa mume ni pamoja na mawazo ya uongozi na miradi.

a) Lazima tutie mkazo kwamba uongozi ni matokeo ya kutumika (tazama Lk. 22:26). Mume si kiongozi wa jamaa yake mpaka awwe mtumu shi wa jamaa yake.

b) Katika Biblia, wongozi na miradi zinaonekana kuwa msimamo wa jukumu ya mwanamume.

c) Katika Mwa 3:20, twaona kwamba mwanamume anachukua msimamo wa kumtaja jina mwanamke. Wale wanaokataa wazo la Kibiblia la wongozi wa mume waweza kubisha na kwamba Adamu angemwuliza Hawa nakumkubali kukata shauri naye.

d) Katika Mwa 3:17, ni wazi kwamba mume lazima aongoze na apeane mwongozo kwa mkewe. Kosa la mwanamume, kulingana na Mungu, ni kwamba badala ya kumwongoza mkewe anamkubali mkewe kumwongoza.

e) Kumbuka, anguko la mwanamume lilikuwa si la kawaida zaidi kuliko kweli kwamba alikula sehemu ya tunda waliloonywa wasile. Mizizi ya kuanguka kwa mwanamume ni hiyo ya kuasi. Mwanamume alikuwa aongoze. Hakufanya hivyo. Mwanamke aliongoza. Waliasi kinyume cha maumbile ya Mungu na mpango wake wa uumbaji.

Maelezo mafupi

2) Tendo la uongozi na lililotangulia ambalo lilipangwaq na Mungu, halipaswi kufanywa kwa nguvu kwa mke. Badala yake, linaimarishwa na upendo.

a) Paulo anaimarisha tofauti hii katika Kol. 3:18,19. Anasema kwamba waume wawapenda wake zao badala ya kuwa na "uchungu" nao.

b) Mume aliye na uchungu na mke wake aweza kujaribu kufanya kwa nguvu uongozi wake kwake. Aweza kukosa kuvumilia kutomjibu na ajaribu kumfanya atii kwa nguvu.

(1) Uongozi huu ambao hujaribu kujitia kwa mtu kwa nguvu si uongozi wa kweli wa Kibiblia.

(2) Uongozi huu unatambuliwa na kiongozi ambaye mara nyingi anakasirishwa na yule anaongoza na mara nyingi analenga makosa ya mtu huyo.

c) Mume ampendaye mke wake ni mvumilivu na hamlaumu. Uongozi wake na miradi yake inapokelewa na mkewe katika kutii.

Tia Maelezo Yako:

Mahali pa Majadiliano

Tumia mawazo ya awali kuendeleza majadiliano juu ya uongozi na kujibu maswali yo yote.

Maelezo mafupi –

d. Tendo kuu la wongozi ni upendo.

1) "Wapendeni wake zenu" (Efe 5:25) ni kwa waume ninyi "watiini waume zenu" (Efe 5:22) ni kwa wake.

a) Kristo na upendo Wake kwa Kanisa ni mfano wa mume.

(1) Ni upendo usio na masharti.

(2) Ni upendo usio na mipaka.

b) Upendo huu lazima uchochewe na ufahamu mkubwa wa umuhimu wa mke. Huu unakubaliana na ufahamu wa Kristo wa umuhimu mkuu wa Kanisa. Unaongoza kwa kutaka kujitoa kwa ajili ya mwingine (Efe 5:25).

c) Upendo huu lazima uwe wa kujitolea uwe sadaka. Lazima wende kwa msalaba.

d) Upendo huu lazima uwe upendo wa huruma. Unapaswa kuwa unakubali ku chukuliana na mkewe kufahamu na kuhusika naye.

(1) Lazima umfanye mume "kutembea katika viatu vyake."

(2) Lazima umwezeshe kumpenda kama mwili wake mwenyewe (Efe 5:28).

2) Maandiko yasema, "alijitoa kwa ajili yake" (Efe 5:25).

a) Huu ni moyo wa upendo "agape".

(1) Kristo alijiletea Kanisa kwa kujitoa yeye mwenyewe.

(2) Adamu alimpata hawa kwa kujitioa yeye mwenyewe (ubavu wake).

(3) Mume humpokea mke kwa kujitoa mwenyewe kwa ajili yake.

b) Hivyo, mwanamume si sana "kujipatia mke" mwenyewe kama anavyojitoa kwa mkewe.

ARUSI

Tia Maelezo Yako:

Maelezo mafupi

Mahali pa Majadiliano

Tumia mawazo ya hapo awali kuendeleza majadiliano juu ya upendo "agape" na ujibu maswali yo yote.

c. Hali ya juu ya uongozi ni kuvumilia na kufahamu.

1) Mume lazima aishi na mkewe kwa akili (tazama 1 Pt 3:7).

a) Lazima afahamu kwamba ni mrithi pamoja naye na kwa hivyo yuko sawasawa naye katika hali ya kufanana katika Kristo.

b) Lazima afahamu pia kwamba yeye ni chombo kisicho na nguvu. Yeye ni wa chini kwake katika mpango wa kuhusiana.

2) Mume amjibu mkewe katika njia ya akili. Hivyo ni, a chukue miradi na aongoze akijua kwamba si jambo la asili kwake kumwongoza.

3) Hii ndiyo sababu ya maombi yako (wingi katika kiyunani) kuzuiliwa katika 1 Pt 3:7.

a) Mume asiyefahamu jukumu la mkewe na hakubali mpango uliowekwa wa mahali pake pa wongozi na Mungu, Hatachukaua mradi wa kuongoza mkewe katika maombi.

b) Mstari waonysha waume na wake ambao hawaombi pamoja kwa sababu mume anakosa kufahamu jukumu za arusi.

ARUSI

Maelezo mafupi

Maelezo ya Mwandishi:

Wakati mwingine hali ya mume ni kwamba anachoka kufanya miradi yote. Anasema: Mbona hawezi kufanya miradi hna kutuongoza katika maombi?

Inachukua mume mwenye nguvu anayefahamu jukumu za arusi kibiblia kuongoza mkewe katika maombi. Hii ni kweli ya uongozi. Twaweza kusema kwamba ni sehemu ngumu ya uongozi.

Ndiyo, waume wana mamlaka, lakinipia wana wajibu! Mume mpole na aliye tayari kutenda ni yule anayehusika sana na wajibu kuliko mamlaka yake.

Mahali pa Majakiliano

Tumia mawazo ya awali kuendeleza majadiliano juu ya haja ya mume kufahamu na kuwa mpole. Pia, jibu maswali yo yote juu ya uongozi.

Tia Maelezo Yako:

ARUSI

D. Kufanana kwa uhusiano wa arusi.

Maelezo mafupi –

Kufanana kwa Arusi #1:

Utatu (tazama 1 Kor 11:3).

Inabaki ikiwa ya muhimu kufahamu kwamba mume na mke hupata usawasawa wao katika mambo ya kufanana kwao katika Kristo, na uongozi wao najukumu za kutii katika mambo ya uhusiano wao mmoja na mwingine.

Jambo hilo hilo ni kweli katika Utatu. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wako sawasawa. Wote ni Mungu. Hata hivyo Mwana humtii Baba. Naye Roho anamtii Mwana.

Msalaba unafunua usawasawa wa wanaume na wanawake (Gal. 3:28). Hata hivyo hauondoi mpango wa Mungu wa uhusiano baina ya mume na mke. Msalaba unafunua usawasawa wa Mwana na Baba unaodumu katika Utatu (Flp 2:6). Hata hivyo hauondoi mpango wa Mungu wa uhusiano katika Utatu (tazama 1 Kor 15:27, 28).

Pia tazama maendeleo ya Biblia yanayoele za Mwana akifanya yale tu anayoyaona Baba akifanya (Yn. 5:19), na Roho akisema tu yale anasikia Mwana akisema (Yn. 16:13, 14). Wanatii mmoja na mwingine katika mpango wa uhusiano, hata hivyo wako sawasawa kabisa katika kufanana.

Hiki ni kinyume cha matarajio ya Utatu. Utatu huu wa Uungu wako sawasawa hata hivyo ni tofauti. Hi pengine, ni kinyume cha matarajio ya arusi pia. Mume na mke wako sawasawa hata hivyo ni tofauti (fikiria wazo la "siri" katika Efe 5:31, 32).

ARUSI

Maelezo mafupi -

Kufanana Kwa Arusi #2:

Uhusiano baina ya Yahweh na Israeli.

Arusi, katika Agano la Kale, ilifunua hali ya uhusiano baina ya M ungu na Israeli.

Kwa kawaida, twaweza kujifunza kitabu cha Wimbo ulio bora wa Sulemanikuona vile kufanana huku kumetumiwa.

Hasa, twaweza kujifunza M anabii ambao mara kwa mara hutazama kufanana huku (fikiria Is 54:1-8; 62:4, 5; Yer 2:2; 3:6-14; 31:32; Eze 16; Ez 23; Hos 1-3; hasa Hos 2:2).

Kufanana Kwa Arusi #3:

Uhusiano baina ya Kristo na Kanisa.

Tume tazama kufanana huku katika kosi hii yote. Kristo ambaye ni Kichwa ni kufanana kwa mume. Kanisa linalotii ni kufanana kwa mke. Kwa kweli, siri hiyo nikubwa (Efe 5:32).

ARUSI

Maelezo mafupi –

E. Maelezo ya mwisho Ya Kosi Yetu.

1. Kristo lazima awe lengo la kila arusi. Kutii na kumpendeza kuwe nia ya utendaji katika jukumu ya arusi yenu.

2. Kuongoza/kutii na uhusiano wa mume na mke lazima usifahamike katika hali yavile mume alivyo na vile mke asivyo. Lazima uangaliwe kama mpango wa Mungu unaokubali kila mwenzi akamilishe mwingine. Kila mwenzi ni wa muhimukama yule mwingine. Kila mwenzi ni wa muhimu kama yule mwingine. Ijapokuwa wao ni sawasawa, hawafanani kabisa.

3. Uhuru wa uke na uume hauimarishwi na kujaribu kuwa vile mmoja asivyo. Wanaumeni wanaume na wanawake ni wanawake. Mwanamume aweza tu kuwa mwanamume aliye huru. Mwanamke aweza kuwa tu mwanamke aliye huru. Kutimiza na uhuru vyapatikana katika mpango wa Mungu wa uhu siano, wala si yake. Kutimiza na uhuru kwa wanaume na wanawake vyapatikana kwa sababu wako sawasawa, si kwa sababu wanafanana.

4. Wakati waume na wake wamekubali na kujizoeza mpango wa Mungu ulioimarishwa na Mungu, basi hawaoni uongozi kama wa kuwekachini na kutii kama utumwa. Wanauona wongozi na kutii kama mlango wazi kwa arusi ya uhuru na raha.

ARUSI

Maelezo mafupi -